
USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI




# ELIMU
# TANZANIA

Ingawa Tanzania imepiga hatua katika upatikanaji na usawa katika elimu, kuna unafuu katika kiwango cha elimu, haswa katika madarasa ya chini. Ustadi wa kusoma unabaki kuwa changamoto miongoni mwa wanafunzi wa Kitanzania. Kwa mfano, takwimu kutoka mikoa minne ya Tanzania bara (Morogoro, Iringa Mtwara na Ruvuma) inaonyesha kwamba ni asilimia 17 mpaka 26 tu ya wanafunzi wa darasa la pili ambao wanaweza kusoma kwa ufahamu. Ugumu unatokana na ukosefu wa rasilimali kwa walimu na wanafunzi: Asilimia 66 ya walimu wenyewe wanaripoti kwamba hawana vifaa vya kutosha darasani kwao kwa ufundishaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Wanafunzi wengi (asilimia 89) huhudhuria darasani ambapo hakuna vifaa vya kusoma vya ziada wakati wa masomo. Wakati uandikishaji wa shule za msingi kati ya wasichana na wavulana ni sawa, ni msichana mmoja tu kati ya watatu wanaoanza shule ya sekondari ndiye atamaliza masomo yao ya sekondari. Sababu za uandikishwaji mdogo kwa wasichana ni pamoja na ugumu wa kiuchumi, ndoa za utotoni na / au mimba zisizotarajiwa, na unyanyasaji wa kijinsia shuleni.

Mwongozo wa elimu wa USAID unafadhili matokeo ya maboresho kwa wanafunzi katika kusoma Kiswahili, lugha ya taifa kwa darasa la kwanza hadi la nne kupitia mradi wake wa Tusome Pamoja. Tusome Pamoja. Ili kufanikisha lengo hili, , USAID inafanya kazi katika ngazi za kitaifa, mkoa, wilaya, na kata kujenga uwezo wa taasisi za serikali za Tanzania kama vile Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia ( na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Serikali (TAMISEMI) juu ya masuala kadhaa ya sera na taasisi. Hii inamaanisha (1) kufanya kazi na wadau muhimu kwenye miongozo ya ualimu, vifaa vya wanafunzi, na mafunzo ya kuzitumia; (2) kujenga uwezo wa kufundisha na kusaidia ushauri kwa walimu; na (3) kukusanya takwimu ambazo zitawezesha kufanya maamuzi kulingana na ushahidi mzuri na utafiti.

Kwa kupitia mfano huu, USAID inatekeleza mradi mpya wa Hesabu na Elimu Jumuishi ili kuboresha ujuzi wa hesabu na kuongeza uwezekano wa kusoma kwa watoto wenye ulemavu katika madarasa ya chini.

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

## ELIMU KWA UJUMLA

### KIWANGO CHA UFADHILI

• Dola za Kimarekani milioni15.5 kwa mwaka wa fedha 2019

### WASHIRIKI WAKUU

• Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia [Tanzania Bara]
• Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali [Zanzibar]
• Ofisi ya Rais, Tawala Bora na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) [Tanzania Bara]
• Ofis ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ [Zanzibar]
• RTI International
• World Education, Inc./ Bantwana Initiative

### ENEO

Tanzania Tanzania Bara
• Morogoro
• Iringa
• Ruvuma
• Mtwara
• Mara
• Arusha

Zanzibar
• Unguja
• Pemba

### MAWASILIANO

Angela Cardenas
acardenas@usaid.gov

USAID pia inasaidia kuongeza uandikishaji wa Watoto wa kike walio katika rika balehe katika shule za sekondari nchini Tanzania kupitia mradi wake wa Waache Wasome. Mradi unafanya kazi kwa karibu na viongozi wa serikali za mitaa, viongozi wa shule na jamii, walimu, na wazazi kuleta mpango kamili wa mikakati kwa shule za sekondari za umma katika wilaya na jamii zilizokusudiwa. Maingiliano haya yameundwa kuwapa uwezo watoto wa kike kuunda na kufikia malengo na mustakabali wa maisha yao na kushughulikia hali za kijamii na vikwazo vya kiuchumi ambavyo vinawalazimisha kubaki na kufanikiwa shuleni. Muingiliano huo unaendelezwa na kutekelezwa sanjari na Mpango wa Serikali wa Kitaifa wa Kitanzania wa kumaliza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

## CHANGAMOTO

• Wingi wa wanafunzi tofauti na ile ya walimu.
• Kuwa na uhakika wa walimu, haswa maeneo ya vijijini.
• Viwango vya ubakizaji wa Watoto wa kike kwa sababu ya umaskini, mimba za utotoni na ndoa, na ukatili wa kijinsia mashuleni
• Ubora wa elimu ya msingi upo chini: ni asilimia 17-26 tu ya wanafunzi wawili wa darasa la pili husoma na kuelewa ufahamu.

## MATOKEO

• Wanafunzi wote wa darasa la kwanza na la pili katika mikoa ya Tusome Pamoja wamepokea vifaa vipya vya kusoma: takriban vifaa vya ziada milioni 1 vimeshasambazwa.
• Walimu wote wa darasa la kwanza na la pili katika mikoa mitano ya Tusome Pamoja (zaidi ya 10,000) wamepata mafunzo juu ya mafunzo ya kusoma kwa madarasa ya chini, kuboresha ujuzi wao na ustadi wao kama waalimu.
• Mchango wa Waache Wasome umechangia asilimia 69 ya wanufaika wa kike kuripoti mwitikio za uwezeshaji, kubadilisha imani kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kupata usawa wa rasilimali za kijamii, kiuchumi na kisiasa na fursa.
• Mfumo wa Onyo la mapema uliotekelezwa na Waache Wasome uliotambulisha wanafunzi wa sekondari 537 ambapo (224) ni watoto wa kike walio hatarini kukatiza masomo yao. Wanafunzi hupokea ushauri nasaha na mwongozo. Walimu hushirikisha wazazi / walezi ili kuhakikisha wanafunzi wanapata msaada shuleni na nyumbani ili wasikatize masomo yao.
• Zaidi ya vikundi 280 vya akiba vinavyolenga akina mama na walezi wa Watoto wa kike wamearifiwa na jumla ya wanachama zaidi ya 6,400. Vikundi hivyo vimeokoa karibu Shilingi za Kitanzania bilioni 1 ($ 435,000) na wametoa mikopo kwa wanachama wa karibu shilngi za Kitanzania bilioni 1.5 ($ 650,000). Vikundi hivyo vimetumia shilingi za Kitanzania milioni 69.5 ($ 30,000) kutoka Mifuko yao ya Elimu kusaidia Watoto wa kike walio hatarini karibu 1,000 walio hatarini na wavulana zaidi ya 700 walio hatarini katika jamii zao ili waweze kuendelea na masomo yao.